

Mwenyezi Mungu alimwita kwake Mbinguni ndugu yetu

Bro. **Meinrad** (Josef) **Heinrich** OSB

kwenye makao yake ya milele tarehe 24 Septemba 2019, saa 2:30 asubuhi kwa utulivu katika nyumba yetu ya kutunzia wagonjwa (Infirmary); ambako alikuwa kwa muda wa miaka miwili.

Bro. Meinrad alizaliwa tarehe 6 Desemba 1934, mjini Illerberg katika Jimbo la Augsburg, nchini Ujerumani. Wazazi wake ni Baba Michael na Mama Fransiska Heinrich. Bro. Meinrad alizaliwa katika familia ya watoto wanne. Wanaume 2 na wanawake wawili yeye akiwa ni mtoto wa mwisho. Alibatizwa na kupewa jina Josef.

Alisoma shule ya msingi kati ya mwaka 1941-1949, katika mazingira magumu ya vita ya pili ya dunia, ambapo Ujerumani ilikuwa uwanja wa vita hiyo. Mwaka 1949 – 1952 alijiunga na chuo cha ufundi cha upakaji rangi huko St. Ottilien. Alifanya mtihani wake wa mwisho na alifaulu vizuri sana. Mwisho alivutwa na maisha ya kitawa na mwaka huo huo 1952 alipokelewa katika upostulanti na unovisi na alifunga nadhiri za kitawa tar 8 June 1954, na mwaka 1957 alifunga nadhiri za daima. Mara baada ya Nadhiri alitumwa Uingereza kujifunza lugha ya Kingereza. Baada ya kufuzu mafunzo hayo ya lugha alitumwa kama Mmisionary nchini Tanzania Abasia ya Peramiho tarehe 22 June 1958.

Kazi ya kwanza kufika Tanzania 1958 ilikuwa ni kujifunza lugha ya Kiswahili hapa Peramiho. Mwaka 1959 alitumwa Parokia ya Lituhi na huko alikuwa chini ya waalimu hodari wa Ujenzi na useremala Bro. Manswetus na Bro. Gabinus ambapo alijifunza kazi ya useremala na ujenzi, kufwatua na kuchoma matofali. Baada ya muda mfupi alikuwa fundi hodari. Mwaka 1959-1969 alitumwa Parokia ya Luilo na alijenga makanisa matatu na majengo ya shule ya msingi. Pia kati ya mwaka 1965-1966 alifanya ukarabati mkubwa wa Parokia ya Lituhi, Chengena, Namabengo na Luganga. Pia alikarabati makanisa ya Ikombe na Lipingu huko Nyasa.

Mwaka 1968 baada ya miaka 10 alipata likizo ya kwanza kwenda Ujerumani. Na alitumia muda wake vizuri kwa kwenda shule ya muziki; alijifunza kucheza kinanda, (Pipes organ) na pia alijifunza kufanya ukarabati wa vinanda vya aina hiyo. Aliporudi mara akawa fundi mkubwa wa kuchiza na kukarabati vinanda vya namna hiyo. Alikarabati vinanda hivyo vikubwa vya hapa Peramiho, kanisa kuu la Kiaskofu Songea, Abasia ya Hanga na Ndanda. Alikuwa na ratiba kila mwaka kufanyia marekebisho vinanda vya namna hiyo. Alifanya kazi hiyo kwa moyo mkubwa na pia alifungua darasa la muziki na kutengeneza vinanda kwa vijana. Bila shaka hata hapa wapo wanafunzi wake.

Miaka ya ya 1971 – 1973 alifanya utume wa ujenzi na ukarabati katika makanisa ya Mahanje, Madaba na Lundu huko Nyasa. Kazi za mwisho alizofanya Bro. Meinrad ni ujenzi wa kanisa la Litapuasi mwaka 1998 na na ukarabati wa paa na kupaka rangi kanisa letu kwa maandalizi ya Jubilei ya miaka 100.

Karibu majimbo yote ya hapa kusini, Songea, Mbinga na Njombe makanisa mengi yamejengwa, kupakwa rangi au kukarabatiwa na Bro. Meinrad kama tulivyoona. Hivyo kwa kifupi tunamshukuru Mungu kwa zawadi ya Bro. Meinrad kuja na kufanya utume kati yetu.

Licha ya kazi hizo zote za kitume Bro. Meinrad hakuwa nyumba katika maisha ya kiroho. Alikuwa mtu wa sala na kushika sana taratibu za maisha ya Jumuia kama mtawa. Alipenda sana unyamavu, tafakari na kusoma maandiko matakatifu na vitabu vya kiroho. Alikuwa na heshima ya pekee kwa Mama Maria hasa kwa kusali Rozari.

Ugonjwa wake

Bro. Meinrad kwa muda mrefu hakuwa na shida ya afya. Kazi zake hasa za ujenzi na kutumia akili kubuni mapaa ya nyumba, kuchanganya rangi na kutembea juu ya mapaa, zinadhihirisha kuhusu hilo. Lakini pole pole kulikuwa na dalili za kupoteza kumbukumbu. Wakati mwingine alionesha wazi hajitambui kuwa yuko wapi. Aliweza kuzungumzia miji ya Ujerumani hali yuko Peramiho. Hayo yalianza kuashiria upotevu mkubwa wa akili na kumbukumbu.

Kuanzia mwaka 2017, ndipo kumbukumbuka zake zilielekea kupungua kabisa na kupelekwa Infirmary. Akiwa Infirmary alipenda sana kusikiliza meledia za Gregorian na pia akisikia wimbo wa “Nampenda Maria” alionesha kuguswa sana. Kwa muda huo mrefu akiwa Infirmary Bro. Meinrad hakuonesha ugonjwa wa pekee. Bali kuanzia Jumapili ya tar 22 Septemba ndipo alipoanza kuonesha kuchoka na kuwa dhaifu. Na tarehe 24 Septemba siku ya Jumanne majira ya saa 2:30 asb Mungu aliichukua Roho yake. Alifariki akiwa na umri wa miaka 85, miaka 65 katika maisha ya kitawa na miaka 61 mmisionari hapa Peramiho - Tanzania.

Shukrani

Tunawashukuru madaktari na wauguzi wote waliomsaidia sana katika ugonjwa wake. Kwa namna ya pekee tunawashukuru wafanyakazi wote wa nyumba yetu ya wagonjwa (infirmary) wakiongozwa na Sr. Pendo OSB, kwa uvumilivu wa kumtunza kwa muda wa miaka 2 hali hajitambui. Tunawashukuru masista wote wa Mtk. Scholastica na wafanyakazi wote waliomtembelea, kusali naye na kumtia moyo katika ugonjwa wake. Pia tunashukuru watawa vijana wa Abasia ya Peramiho maana walijiwekea utaratibu wa kumtunza na kumhudumia mzee wetu. Hata mara moja hatukusikia wakilalamika. Maandiko yanatuambia unalotaka kutendewa mtendee mwenzako hivo hivo. Tunatumaini walivomhudumia mzee wetu nao watahudumiwa hivyo hivyo.

Mwenyezi Mungu ampokee katika utukufu wake na hasa kutokana na utume wake wa kutukuka wa ujenzi wa makanisa na nyumba za kanisa.

Raha ya milele umpe Ee Bwana ..... astarehe kwa Amani. Amina

Pd. Sylvanus Kessy OSB, Prior Msimamizi
Na watawa wa Abasia ya Peramiho
27.09.2019